JAMHURI YA KENYA
WIZARA YA ELIMU
Mali ya serikali ya Kenya
HAUUZWI

# MTAALA WA DARAJA YA JUU YA SHULE ZA UPILI

## GREDI YA 10

# FASIHI YA KISWAHILI

TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA
2024

DRAFT

**TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**

# MTAALA WA DARAJA YA JUU YA SHULE YA UPILI

# GREDI YA 10

# FASIHI YA KISWAHILI

**JUNI, 2024**

DRAFT

Toleo la Kwanza 2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtaala huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

**ISBN: 978-9914-52-929-6**

Kimechapishwa na kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya

**YALIYOMO**

YALIYOMO .... i
MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA .... ii
MATOKEO YA DARAJA YA JUU YA ELIMU YA MSINGI .... iv
ORODHA YA MASOMO YALIYOPENDEKEZWA KATIKA DARAJA YA JUU YA SHULE ZA UPILI. .... vi
MGAO WA VIPINDI KATIKA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI .... vii
KAULI KIINI .... vii
MATOKEO MAALUM YA KIJUMLA YA DARAJA YA JUU YA SHULE ZA UPILI .... viii
MUHTASARI WA MADA NA MADA NDOGO .... ix
MADA NA MADA NDOGO .... 1
VIGEZO NA VIWANGO VYA KUZINGATIA KATIKA KUTATHMINI .... 62

DRAFT

## MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA

Elimu nchini Kenya inatakiwa:

1. **Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa**
   Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kuondoa mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana. Mielekeo hii itawawezesha wanajamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia ukuaji wa taifa.

2. **Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa**
   Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa taifa la Kenya kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.
   **a) Mahitaji ya kijamii**
   Elimu nchini Kenya lazima iwatayarishe vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mageuzi taratibu ya kijamii kutokana na maendeleo ya haraka ya usasa. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kujirekekebisha kutokana na mabadiliko haya.
   **b) Mahitaji ya kiuchumi**
   Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na sifa za kibinafsi zinazohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika humu nchini.
   **c) Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda**
   Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda. Kenya inatambua mabadiliko ya haraka ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunaweza kuwa sehemu ya maendeleo haya ikiwa mfumo wetu wa elimu utalenga kimakusudi maarifa, stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko ya yanayoendelea ulimwenguni.

3. **Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza**
   Elimu inapaswa kuwezesha kutambua, kukuza na kuimarisha vipawa vya kila mmoja ili kuweza kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

4. **Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini**
   Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.

5. **Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji**
   Usawa wa kijamii kwa mfano, usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa.
   Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zenye changamoto zitakazowawezesha kutoa huduma jumuishi za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.

6. **Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya**
   Elimu inafaa kuwapa vijana uelewa wa tamaduni za kale na za sasa na nafasi yazo katika jamii ya kisasa. Vijana wanafaa kuambatanisha maadili ya tamaduni bora na mahitaji yanayobadilika kulingana na maendeleo yanayotokea ili kujenga jamii thabiti ya kisasa.

7. **Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine**
   Kenya kama nchi mojawapo ya jamii ya kimataifa inakusudia elimu iwaelekeze Wakenya kutambua na kuthamini mahusiano ya kimataifa kwa kuzingatia mikataba, uwajibikaji, haki na manufaa yanayoambatana na ushirika huo.

8. **Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira**
   Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Aidha, inafaa kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira na kuwaelekeza vijana kuthamini usafi wa mazingira.

DRAFT

## MATOKEO YA DARAJA YA JUU YA ELIMU YA MSINGI

Kufikia mwisho wa Daraja ya Juu Shule ya Upili, mwanafunzi aweze:

1. kuwasiliana kikamilifu na kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika miktadha mbalimbali
2. kutumia ujuzi wa kihisabati, kimantiki na uwazaji kina katika utatuzi wa matatizo
3. kutumia ujuzi wa kimsingi wa kiutafiti na kisayansi kuboresha mazingira yake na kutatua matatizo mbalimbali
4. kutambua na kutumia kipaji chake katika burudani, kujitosheleza na kujiendeleza kielimu na kitaaluma
5. kudumisha maadili ya kitaifa na kidini na kuyatumia katika shughuli za kila siku
6. kutumia na kukuza mikakati ya kiafya katika shughuli za kila siku
7. kutunza, kuhifadhi na kuboresha mazingira ili kujikimu maishani
8. kudhihirisha uraia wa kitaifa na kimataifa kwa ajili ya utangamano na ushirikiano
9. kuthamini tofauti za kijamii na tamaduni mbalimbali
10. kuwajibika katika kudhibiti masuala mtambuko.

DRAFT

## DARAJA YA JUU YA SHULE ZA UPILI KATIKA MTAALA WA KIUMILISI

Daraja ya Juu ya Shule za Upili ndiyo kiwango cha nne cha Elimu ya Msingi katika Mtaala wa Kiumilisi kitakachofikiwa na wanafunzi baada ya kupitia chekechea, shule ya msingi na shule ya junia. Kiini cha Daraja ya Juu Shule za Upili ni kuwapa wanafunzi mafunzo kabla ya kujiunga na vyuo vikuu vilevile kupata tajriba kabla ya kujiunga na ulimwengu wa kazi ambapo wanafunzi watapata fursa ya kuchagua mkondo ambao wameupendelea au kuonyesha kuwa na uwezo nao hapo awali. Daraja ya Juu ya Shule za Upili huhusisha mafunzo ya miaka mitatu kwa wanafunzi kati ya miaka 15 hadi 18 na kuweka msingi wa elimu na mafunzo katika ngazi ya elimu ya juu na pia ulimwengu wa kazi. Katika Ruwaza ya Mtaala wa Kiumilisi, wanafunzi wanaokamilisha kiwango hiki wanatarajiwa kuhusishwa, uwezeshwa na pia mnye maadili tayari kushiriki katika maendeleo ya kiuchumi ya taifa.

Katika kiwango hiki, wanafunzi watachagua masomo saba (7) kama ilivyopendekezwa na tume ya rais ya elimu. Hii itahusisha **masomo manne** ya lazima na **matatu** ambayo mwanafunzi atachagua kulingana na mkondo aliochagua. Ingawa English na Kiswahili yameorodheshwa kama masomo la lazima, wanafunzi ambao watachagua masomo haya kama masomo maalum watafuata mtaala tofauti kwa upande wa upeo, shughuli za ujifunzaji na tathmini. Kwa hivyo, wanafunzi hawa watachukua Advanced English au Kiswahili Kipevu pamoja na masomo mengine mawili. Inapendekezwa kwamba angalau **masomo mawili** ya ujifunzaji yanapaswa kutoka kwa mkondo aliouchagua. Katika hali ya kipekee, baadhi ya wanafunzi wanaweza kuchagua somo moja kutoka mkondo waliouchagua na upeo wa **Masomo Mawili** kutoka kwa mojawapo ya mikondo mitatu, kutegemea makadirio mwanafunzi ya kazi na maelekezo ya mwalimu mkuu wa Daraja ya Juu ya Shule ya Upili.

**ORODHA YA MASOMO YALIYOPENDEKEZWA KATIKA DARAJA YA JUU YA SHULE ZA UPILI.**

| **Masomo Ya Lazima** | **Science, Technology, Engineering & Mathematics (STEM)** | **Social Sciences** | **Arts & Sports Science** |
| --- | --- | --- | --- |
| 1. English<br>2. Kiswahili/KSL<br>3. Community Service Learning<br>4. Physical Education<br><br>*Tanbihi; Kila mwanafunzi atapata fursa ya kupata ujuzi wa kidijitali ili kufanikisha ujifunzaji na pia kujifurahisha/kujiburudisha* | 5. Mathematics/Advanced Mathematics<br>6. Biology<br>7. Chemistry<br>8. Physics<br>9. General Science<br>10. Agriculture<br>11. Computer Studies<br>12. Home Science<br>13. Drawing and Design<br>14. Aviation Technology<br>15. Building and Construction<br>16. Electrical Technology<br>17. Metal Technology<br>18. Power Mechanics<br>19. Wood Technology<br>20. Media Technology*<br>21. Marine and Fisheries Technology* | 22. Advanced English<br>23. Literature in English<br>24. Indigenous Language<br>25. Kiswahili Kipevu/Kenya Sign Language<br>26. Fasihi ya Kiswahili<br>27. Sign Language<br>28. Arabic<br>29. French<br>30. German<br>31. Mandarin Chinese<br>32. History and Citizenship<br>33. Geography<br>34. Christian Religious Education/ Islamic Religious Education/Hindu Religious Education<br>35. Business Studies | 36. Sports and Recreation<br>37. *Physical Education (C)*<br>38. Music and Dance<br>39. Theatre and Film<br>40. Fine Arts |

DRAFT

## MGAO WA VIPINDI KATIKA DARAJA YA JUU SHULE ZA UPILI

Idadi ya vipindi katika masomo ya lazima vitakuwa vinne (4); ilhali vipindi vya masomo ambayo sio ya lazima vitakuwa sita (6). Kila kipindi kitakuwa dakika arobaini (40). Vipindi huru vitatumiwa kukuza ujuzi wa kidijitali, program za maelekezo ya kidini, miradi, kusoma kiushirikiano na mafunzo ya kiada.

## KAULI KIINI

Somo la Fasihi ya Kiswahili katika kiwango hiki linaendeleza maarifa aliyoyapata mwanafunzi katika daraja ya awali ya masomo ya sekondari. Ni dhahiri kuwa fasihi iliyoandikwa katika lugha lengwa inaweza kuwapa wanafunzi ufahamu wa tamaduni za lugha zingine, hivyo kuwaandaa kutenda kwa umilisi na ufanisi katika kutangamana na watu wa tamaduni hizo.

Fasihi ya Kiswahili inajumuisha uchanganuzi wa fasihi simulizi, uhakiki wa fasihi andishi na uzalishaji na uwasilishaji wa kazi za fasihi. Kupitia tanzu hizi, fasihi itaimarisha umoja wa watu wa tamaduni mbalimbali na kuchangia uwiano na utangamano wa kitaifa. Somo hili litampa mwanafunzi msisimko wa kutathmini, kufurahia na kuhakiki tanzu mbalimbali za fasihi andishi na fasihi simulizi. Kupitia uchambuzi wa tanzu mbalimbali kwa kuzingatia vigezo kama uhusika, maudhui, mtiririko, mandhari na mbinu za uandishi, mwanafunzi atapata mitazamo tofauti kuhusu ulimwengu na kukuza ari ya kutunga kazi za fasihi. Umaarufu wa kazi za fasihi umechochewa na hatua ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kuitangaza rasmi siku ya Kiswahili duniani (tarehe 7 Julai kila mwaka) mwaka 2021, Muungano wa Afrika kukitambua Kiswahili kama lugha rasmi mnamo mwaka wa 2022 na Jumuia ya Afrika Mashariki kukitambua Kiswahili kama lugha ya kanda ya Afrika Mashariki na Kati.

Wanafunzi watapata nafasi ya kutazama kazi za kifasihi zilizoigizwa, kushiriki katika mijadala kuhusu kazi za fasihi zilizoandikwa na kuhusishwa katika tamasha za muziki na maigizo. Aidha, watatafiti na kuandika kazi mradi juu ya fasihi simulizi na kushiriki katika mijadala kati ya shule mbalimbali kuhusu matini teule za fasihi. Somo hili litamwandaa

mwanafunzi kwa mafunzo katika ngazi ya juu pamoja na kujenga stadi zinazohitajika katika taaluma kama vile uanahabari, uandishi, sanaa za kitamaduni na uwanda wa burudani.

## MATOKEO MAALUM YA KIJUMLA YA DARAJA YA JUU YA SHULE ZA UPILI

Kufikia mwisho wa Daraja ya Juu ya Shule za Upili,mwanafunzi aweze:

1. kuwasiliana ipasavyo na kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika miktadha mbalimbali.
2. kutumia maarifa ya kihisabati, kimantiki na uwazaji kina katika utatuzi wa matatizo.
3. kutumia maarifa ya kimsingi ya utafiti na sayansi kuboresha mazingira yake na kutatua matatizo mbalimbali.
4. kutumia vizuri vipaji mbalimbali kwa ajili ya burudani, kujiendeleza kitaaluma, kielimu pamoja na kimafunzo.
5. kudumisha tunu za kitaifa, kimaadili na kidini katika maisha ya kila siku.
6. kutumia na kuendeleza mikakati ya matunzo ya kiafya katika maisha ya kila siku.
7. kulinda, kuhifadhi na kuboresha mazingira kwa ajili ya uendelevu.
8. kudhihirisha uraia wa kitaifa na wa kimataifa kwa ajili ya utangamano wa kidugu.
9. kuonyesha uthamini wa tofauti za watu na tamaduni.
10. kuonyesha uwajibikaji katika kushughulikia masuala mtambuko.

DRAFT

## MUHTASARI WA MADA NA MADA NDOGO

| Mada | Mada Ndogo | Idadi ya Vipindi Vilivyopendekezwa |
|---|---|---|
| **Fasihi Simulizi** | 1.1.1 Misingi ya fasihi simulizi | 6 |
| | 2.1.1 Hadithi: hekaya na hurafa | 2 |
| | 3.1.1 Semi: utangulizi | 4 |
| | 4.1.1 Ushairi simulizi: utangulizi | 4 |
| | 5.1.1 Mazungumzo: utangulizi | 8 |
| | 6.1.1 Maigizo: utangulizi | 6 |
| | 7.1.1 Hadithi: Ngano za mazimwi na mighani | 4 |
| | 8.1.1 Semi: misemo na nahau | 4 |
| | 9.1.1 Nyimbo: utangulizi | 4 |
| | 10.1.1 Ushairi simulizi: maghani ya kawaida | 6 |
| **Ushairi** | 1.2.1 Uainishaji wa Mashairi: utangulizi | 3 |
| | 2.2.1 Makundi ya mashairi : huru na ya arudhi | 4 |

DRAFT

| | | |
|---|---|---|
| | 3.2.1 Uchambuzi wa mashairi: maudhui na dhamira | 4 |
| | 4.2.1 Uchambuzi wa mashairi: maudhui na dhamira | 2 |
| | 5.2.1 Ushairi: mandhari na wahusika | 6 |
| | 6.2.1 Uchambuzi wa ushairi: utangulizi | 5 |
| | 7 .2.1 Ushairi: mbinu za lugha | 4 |
| | 8.2.1 Ushairi: mbinu za lugha | 4 |
| | 9.2.1 Uchambuzi wa ushairi: uhuru wa mshairi | 5 |
| | 10.2.1 Uchambuzi wa ushairi: uhuru wa mshairi | 3 |
| **Bunilizi** | 1.3.1 Utangulizi wa Bunilizi | 6 |
| | 2.3.1 Tamthilia: maudhui na dhamira | 10 |
| | 3.3.1 Tamthilia: wahusika na mandhari | 10 |
| | 4.3.1 Tamthilia: muundo na mtindo | 12 |
| | 5.3.1 Tamthilia: muundo na mtindo | 12 |
| | 6.3.1 Riwaya: maudhui na dhamira | 10 |

DRAFT

| | | |
|---|---|---|
| | 7.3.1 Riwaya: wahusika na mandhari | 10 |
| | 8.3.1 Riwaya: muundo na mtindo | 8 |
| | 9.3.1 Riwaya: muundo na mtindo | 8 |
| | 10.3.1 utunzi wa fasihi bunilizi | 4 |
| | | **178** |

DRAFT

## MADA NA MADA NDOGO

<table>
<tr><td colspan="5">1.0</td></tr>
<tr><td>Mada</td><td>Mada Ndogo</td><td>Matokeo Maalum Yanayotarajiwa</td><td>Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa</td><td>Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa</td></tr>
<tr><td>1.1 Fasihi Simulizi</td><td>1.1.1 Utangulizi wa Fasihi Simulizi<br><br>(Vipindi 6)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya fasihi ili kuibainisha,<br>b) kueleza maana ya fasihi simulizi ili kuibainisha,<br>c) kufafanua sifa za fasihi simulizi,<br>d) kujadili umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii,<br>e) kuchangamkia fasihi simulizi katika jamii.</td><td>Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya fasihi,<br>• kueleza maana ya fasihi simulizi,<br>• kufafanua sifa za fasihi simulizi ili kuzibainisha,<br>• kutumia kifaa cha kidijitali kutafiti sifa za fasihi simulizi,<br>• kusikiliza kanda iliyorekodiwa kuhusu fasihi simulizi ili kufafanua sifa zake,<br>• kushirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii.</td><td>1. Je, ni mambo yapi unayoyafahamu kuhusu fasihi simulizi?<br>2. Je, fasihi simulizi ina umuhimu gani katika jamii?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili sifa za Fasihi Simulizi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidjitali kutafiti sifa za Fasihi Simulizi.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anaposikiliza na fafanua sifa za Fasihi Simulizi katika jamii.</td></tr>
</table>

DRAFT

| |
|---|
| • Kujiamini: mwanafunzi anapojadili ipasavyo kuhusu sifa za Fasihi Simulizi anaposhirikiana na wenzake. |
| **Maadili:**<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotummia vifaa vya kidijitali kusakura mtandaoni.<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa Fasihi simulizi katika jamii.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa Fasihi simulizi katika jamii.<br>• Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa Fasihi simulizi katika jamii. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapojadili umuhimu wa Fasihi simulizi katika jamii.<br>• Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotumia mtandao salama kutafiti kuhusu sifa za Fasihi simulizi. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **1.2 Ushairi** | **1.2.1 Uainishaji wa Mashairi**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya ushairi ili kuupambanua,<br>b) kujadili sifa za ushairi kama utanzu wa fasihi,<br>c) kuchambua sifa za ushairi katika mashairi mbalimbali,<br>d) kufafanua dhima ya ushairi katika jamii,<br>e) kuchangamkia aina mbalimbali za mashairi katika jamii. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya ushairi,<br>• kutafiti mtandaoni au katika matini andishi sifa za ushairi,<br>• kuwawasilishia wenzake matokeo ya utafiti aliofanya,<br>• kujadili sifa za ushairi,<br>• kuchambua sifa za ushairi katika mashairi,<br>• kufafanua dhima ya ushairi,<br>• kuimba na kukariri mashairi mbalimbali. | 1. Ni mambo gani yanayokufanya utambue shairi kama utungo wa fasihi?<br>2. Mashairi yana umuhimu gani kwako? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano - mwanafunzi anaposhiriki majadiliano na wenzake kuhusu s.
- Ujuzi wa kidijitali - mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidjitali kutafiti sifa za ushairi.
- Uwazaji kina - mwanafunzi anapofafanua dhima ya ushairi katika jamii.
- Kujiamini - anapojadili ipasavyo kuhusu sifa za ushairi.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima - mwanafunzi anapowasikiliza wenzake na kuthamini michango yao katika kujadili sifa za ushairi.<br>• Amani - mwanafunzi anaposhirikiana vizuri na wenzake katika kujadili sifa za ushairi.<br>• Uwajibikaji - mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu sifa za ushairi na kutunza kifaa cha kudijitali.<br>• Umoja - mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kijadili sifa za ushairi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala mtambuko anuwai kutokana na mashairi mbalimbali. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.3 Bunilizi** | **1.3.1 Utangulizi wa Bunilizi**<br><br>(Vipindi 6) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya bunilizi ili kuibainisha,<br>b) kujadili aina za bunilizi ili kuzibainisha,<br>c) kujadili vipengele vya bunilizi,<br>d) kuchangamkia usomaji wa bunilizi katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya bunilizi,<br>• kujadili aina za bunilizi,<br>• kutafiti maktabani na kusakura mtandaoni ili kubainisha aina za bunilizi,<br>• kuwasilisha matokeo ya utafiti wake kwa wenzake ili wayatolee maoni,<br>• kusilikiliza aina mbalimbali za bunilizi zilizorekodiwa kwenye kinasa sauti,<br>• kupambanua aina mbalimbali za bunilizi,<br>• kushirikiana na wenzake kujadili vipengele vya bunilizi. | 1. Ni aina gani za bunilizi ulizowahi kusoma?<br>2. Kwa nini ni muhimu kusoma bunilizi? |

DRAFT

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowasilisha matokeo ya utafiti wake kwa wenzake ili wayatolee maoni.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowawasilishia wenzake matokeo ya utafiti wake ili wayatolee maoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoeleza ujumbe wa matini aliyosoma.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti maktabani na mtandaoni iili kubainisha aina za fasihi bunilizi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi kutafiti anaposakura mtandaoni ili kubainisha aina za fasihi bunilizi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapotoa maoni kwa heshima kuhusu uwasilishaji wa wenzake kuhusu aina za fasihi bunilizi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anaposakura kwenye mtandao salama ili kupata aina za fasihi bunilizi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi akitumia msamiati aliojifunza.

**Masuala Mtambuko:**

Kujiamini: mwanafunzi anapowasilisha kwa ujasiri matokeo ya utafiti wake kuhusu aina za fasihi bunilizi.

DRAFT

| **2.0** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
| **2.1 Fasihi Simulizi** | **2.1.1 Hadithi**<br>- *Hekaya*<br>- *Hurafa*<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya hadithi ili kuibainisha,<br>b) kueleza maana ya hekaya na hurafa ili kuzibainisha,<br>c) kufafanua sifa za hekaya na hurafa ili kuzipambanua,<br>d) kujadili umuhimu wa hekaya na hurafa katika jamii,<br>e) kuwasilisha hekaya na hurafa akizingatia vipengele vya uwasilishaji,<br>f) kuchangamkia masimulizi ya hekaya na hurafa katika jamii. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya hekaya na hurafa,<br>• kufafanua sifa za hekaya na hurafa,<br>• kushirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa hekaya na hurafa,<br>• kujadili vipengele vya uwasilishaji wa hekaya na hurafa,<br>• kumsikiliza mgeni mwalikwa akiwasilisha hekaya na hurafa,<br>• kusikiliza na kutazama hekaya na hurafa zikiwasilishwa mtandaoni,<br>• kuwawasilishia wenzake hekaya na hurafa. | 1. Ni aina gani za hadithi za fasihi simulizi unazozijua?<br>2. Je, hadithi zina umuhimu gani katika jamii? |

DRAFT

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa hadithi.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapofafanua sifa za hekaya na hurafa.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anaposimulia hekaya na hurafa. |
| **Maadili:**<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa semi katika Fasihi Simulizi.<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapojadiliana. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposimulia hekaya na hurafa kutoka jamii mbalimbali. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.2 Ushairi** | **2.2.1 Uchambuzi wa Mashairi**<br>*Makundi ya Mashairi*<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana za ushairi arudhi na ushairi huru ili kuzipambanua,<br>b) kujadili sifa za ushairi arudhi na ushairi huru,<br>c) kutambua mashairi arudhi na mashairi huru katika matini,<br>d) kuchangamkia makundi makuu ya ushairi katika fasihi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya ushairi arudhi na ushairi huru,<br>• kutafiti mtandaoni au katika matini andishi sifa za ushairi arudhi na ushairi huru,<br>• kujadili sifa za mashairi arudhi na huru,<br>• kulinganisha na kulinganua sifa za ushairi arudhi na ushairi huru,<br>• kutambua mashairi arudhi na huru katika matini mbalimbali. | 1. Mashairi uliyowahi kusoma ni ya aina gani?<br>2. Mashairi uliyowahi kusoma yana sifa gani? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kujadili na wenzake sifa za mashairi arudhi na huru.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidjitali kutafiti sifa za ushairi arudhi na huru.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotofautisha mashairi arudhi na huru katika matini.
- Kujiamini: mwanafunzi anapojadili ipasavyo kuhusu sifa za mashairi arudhi na huru.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima:  mwanafunzi anapowasikiliza wenzake na kuthamini michango yao katika kujadili sifa za mashairi huru na ya arudhi.<br>• Amani: mwanafunzi anaposhirikiana vizuri na wenzake katika kujadili sifa za mashairi huru na ya arudhi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu sifa za mashairi ya arudhi na huru na kutunza kifaa cha kidijitali.<br>• Umoja : mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili sifa za mashairi arudhi na huru.. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala mtambuko anuwai kutokana na mashairi mbalimbali. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.3 Bunilizi** | **2.3.1 Tamthilia**<br>-*Maudhui*<br>-*Dhamira*<br><br>(Vipindi 10) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya maudhui na dhamira katika fasihi,<br>b) kujadili maudhui na dhamira katika tamthilia teule,<br>c) kuchambua maudhui na dhamira katika tamthilia teule,<br>d) kuchangamkia maudhui na dhamira katika tamthilia mbalimbali. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya maudhui katika fasihi,<br>• kutambua maudhui na dhamira mbalimbali katika tamthilia teule,<br>• kujadili na wenzake maudhui na dhamira ya tamthilia teule,<br>• kuwawasilishia wenzake darasani uchambuzi wake kuhusu maudhui,<br>• kuandika maelezo mafupi kuhusu maudhui katika tamthilia teule. | 1. Tamthilia ulizowahi kusoma zina ujumbe gani?<br>2. Watunzi huchochewa na mambo gani wanapoandika tamthilia? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kujadili dhamira na maudhui katika tamthilia.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowawasilishia wenzake ufupisho wa dhamira na maudhui ili waujadili na kutolea maoni.
- Uwazaji kina: mwanafunzi anapochanganua maudhui na dhamira katika tamthilia na kuwasilishia wenzake.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapodhamini maoni ya wenzake wanapotambua na kujadili dhamira na maudhui katika tamthilia.<br>• Umoja: mwanafunzi anapotagusana na wengine ili kutambua na kujadili dhamira na maudhui katika tamthilia. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala mtambuko anuwai: mwanafunzi anapochanganua maudhui mbalimbali katika tamthilia. |

DRAFT

**3.0**

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.1 Fasihi Simulizi** | **3.1.1 Semi**<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya semi katika fasihi simulizi,<br>b) kufafanua sifa za semi katika fasihi simulizi,<br>c) kujadili umuhimu wa semi katika jamii,<br>d) kuainisha vipera vya semi ili kuvibainisha,<br>e) kufurahia matumizi ya vipera mbalimbali vya semi katika fasihi simulizi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya semi katika fasihi simulizi,<br>• kutumia vifaa vya kidijitali kusakura aina mbalimbali za semi,<br>• kutambua semi katika tungo za fasihi simulizi,<br>• kueleza sifa za semi katika tungo za fasihi simulizi,<br>• kushirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa semi katika fasihi simulizi. | 1. Je, unafahamu aina zipi za semi katika fasihi simulizi?<br>2. Semi zina manufaa gani katika jamii? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusakura aina mbalimbali za semi.
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikian na wenzake kujadili umuhimu wa semi katika Fasihi Simulizi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua sifa za semi katika Fasihi Simulizi.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Umoja : mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa semi katika Fasihi Simulizi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojadili na wenzake umuhimu wa semi katika Fasihi Simulizi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Usalama wa mtandaoni: mwanafunzi anapotumia mtandao salama kusakura aina mbalimbali za semi.<br>• Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa semi katika Fasihi Simulizi. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.2 Ushairi** | **3.2.1 Uchambuzi wa Maudhui na Dhamira**<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana za maudhui na dhamira ili kuzibainisha,<br>b) kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi,<br>c) kufurahia kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya maudhui na dhamira,<br>• kutafiti mtandaoni au katika matini andishi maana ya maudhui na dhamira,<br>• kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi,<br>• kuwasilisha darasani maudhui na dhamira katika mashairi aliyosoma,<br>• kutathmini mawasilisho ya wenzake kuhusu maudhui na dhamira. | 1. Mashairi uliyowahi kusoma yana ujumbe gani?<br>2. Maudhui na dhamira yanajitokeza vipi katika mashairi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasilisha ipasavyo maudhui na dhamira katika mashairi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu maana ya maudhui na dhamira.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu maudhui na dhamira.

**Maadili:**
- Heshima: mwanafunzi anapowasikiliza wenzake na kuthamini michango yao katika kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana vizuri na wenzake katika kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi.

DRAFT

| |
|---|
| • Uwajibikaji: mwanafunzi anapochambua maudhui na dhamira katika mashairi na kutunza kifaa cha kidijitali. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Mwanafunzi anaposoma mashairi anuwai. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.3 Bunilizi** | **3.3.1 Tamthilia**<br>- *Wahusika*<br>- *Mandhari*<br><br>(Vipindi 10) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya wahusika na mandhari katika tamthilia teule,<br>b) kutambua wahusika na mandhari katika tamthilia teule,<br>c) kujadili sifa za wahusika katika tamthilia teule,<br>d) kueleza umuhimu wa wahusika na mandhari katika tamthilia teule,<br>e) kujadili mbinu za usawiri wahusika katika tamthilia teule,<br>f) kujadili mafunzo yanayotokana na matendo ya wahusika katika tamthilia, | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya wahusika na dhamira,<br>• kutambua wahusika na mandhari katika tamthilia teule,<br>• kujadili mbinu za usawiri wa wahusika katika tamthilia,<br>• kujadili sifa za wahusika katika tamthilia teule,<br>• kujadili uhalisia wa wahusika katika jamii yake,<br>• kuchanganua umuhimu wa wahusika katika tamthilia teule,<br>• kutafiti mtandaoni au katika matini andishi maelezo kuhusu mandhari na wahusika na kujadili na wenzake, | 1. Ni nini humchochea mwandishi wa tamthilia anapoteua wahusika wake?<br>2. Mahali na wakati unaorejelewa katika tamthilia huwa na umuhimu gani? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td>g) kuchangamkia nafasi ya wahusika na mandhari katika tamthilia.</td><td><ul><li>kutathmini maelezo ya wenzake kuhusu mandhari na wahusika,</li><li>kuchambua mandhari katika tamthilia teule.</li></ul></td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<ul><li>Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoeleza wenzake kwa ufasaha kuhusu dhana ya mandhari katika tamthilia.</li><li>Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni au katika matini andishi maelezo kuhusu mandhari na wahusika.</li><li>Kujiamini: mwanafunzi anapojadili na wenzake na kuchangia kikamilifu maelezo kuhusu mandhari na kutathmini maelezo yao.</li><li>Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni na kusoma maelezo kuhusu mandhari na wahusika katika tamthilia.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<ul><li>Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuchambua mandhari katika tamthilia teule.</li><li>Heshima: mwanafunzi anapotathmini maelezo ya wenzake kuhusu mandhari na wahusika.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala Mtambuko:<br>Kujiamini: mwanafunzi anapowasilisha maoni yake kuhusu wahusika na mandharikwa wenzake kwa ujasiri.</td></tr>
</table>

DRAFT

| **4.0** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **4.1 Fasihi Simulizi** | **4.1.1 Ushairi Simulizi**<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya ushairi simulizi ili kuubainisha,<br>b) kufafanua sifa za ushairi simulizi ili kuzipambanua,<br>c) kuchambua sifa za ushairi simulizi katika simulizi,<br>d) kujadili dhima za ushairi simulizi katika jamii,<br>e) kuchangamkia ushairi simulizi katika jamii. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya ushairi simulizi,<br>• kutaja vipera mbalimbali vya ushairi simulizi,<br>• kusoma matini andishi au kusikiliza mashairi yaliyorekodiwa,<br>• kumsikiliza mgeni mwalikwa akiimba au kughani ushairi simulizi na kutambua sifa zinazojitokeza,<br>• kutafiti mtandaoni sifa za ushairi simulizi,<br>• kufafanua sifa za ushairi simulizi,<br>• kuchambua sifa za ushairi simulizi katika simulizi,<br>• kushirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa ushairi simulizi. | Kuna umuhimu gani kujifunza ushairi simulizi? |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa ushairi simulizi.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapowasilisha vipera mbalimbali vya ushairi simulizi kwa wenzake.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapowasilisha vipera mbalimbali vya ushairi simulizi. | | | | |

DRAFT

- Uraia: mwanafunzi anapojadili umuhimu wa ushairi simulizi katika jamii yake.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasilisha vipera mbali mbali vya ushairi simulizi.

**Maadili:**
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa ushairi simulizi.
- Heshima: mwanafunzi anapoyathamini maoni ya wenzake wanapojadiliana.

**Masuala Mtambuko:**
- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapowasilisha vipera mbalimbali vya ushairi simulizi.
- Maswala ya elimu ya uraia: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu umuhimu wa ushairi simulizi katika jamii.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Ushairi** | **4.2.1 Uchambuzi wa Maudhui na Dhamira** (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi,<br>b) kulinganisha na kulinganua maudhui na dhamira katika mashairi mbalimbali,<br>c) kufurahia maudhui na dhamira katika mashairi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi,<br>• kulinganisha na kulinganua maudhui na dhamira katika mashairi mbalimbali,<br>• kusoma mashairi mtandaoni na kuchambua maudhui na dhamira yake,<br>• kuwawasilishia wenzake maudhui na dhamira aliyochambua katika matini ya ushairi. | 1. Kuna maudhui gani katika mashairi uliyowahi kusoma?<br>2. Kuna dhamira gani katika mashairi uliyowahi kusoma? |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Kujiamini:mwanafunzi anapowasilisha ipasavyo maudhui na dhamira katika mashairi.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu maana ya maudhui na dhamira.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapolinganisha na kulinganua maudhui na dhamira katika mashairi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposoma na kuchambua maudhui na dhamira ya mashairi mtandaoni. | | | | |
| **Maadili:**<br>• Amani: mwanafunzi anapohusiana vizuri na wenzake wakati wa kuchambua maudhui na dhamira katika mashairi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapochambua maudhui na dhamira katika mashairi na kutunza kifaa cha kidijitali.<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu maudhui na dhamira. | | | | |

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala mtambuko anuai katika mashairi mbalimbali. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.3 Bunilizi** | **4.3.1 Tamthilia**<br>- *Muundo*<br>- *Mtindo*<br><br>( Vipindi 12) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya muundo na mtindo katika tamthilia,<br>b) kutambua vipengele vya muundo na mtindo katika tamthilia,<br>c) kujadili vipengele vya muundo na mtindo katika tamthilia teule,<br>d) kutathmini nafasi ya vipengele vya muundo na mtindo katika tamthilia teule,<br>e) kuchambua tamthilia teule kwa kuzingatia muundo na mtindo wake,<br>f) kuonea fahari muundo na mtindo katika tamthilia. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kufafanua maana ya muundo na mtindo katika tamthilia,<br>• kufanya utafiti mtandaoni au katika matini andishi kuhusu vipengele vya muundo na mtindo wa tamthilia na kuwawasilishia wenzake,<br>• kuigiza sehemu za tamthilia teule darasani,<br>• kutathmini kazi iliyowasilishwa na wenzake darasani kuhusu vipengele vya muundo na mtindo wa tamthilia,<br>• kutazama video ya mchezo wa kuigiza na kujadili vipengele vya muundo na mtindo,<br>• kujadili vipengele vya muundo na mtindo katika tamthilia teule darasani, | 1. Je, tamthilia huwa na mpangilio gani?<br>2. Vipengele vya mtindo na muundo vina umuhimu gani katika tamthilia? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kuchambua tamthilia teule kwa kuzingatia vipengele vya muundo na mtindo,<br>• kutathmini nafasi ya vipengele vya muundo na mtindo katika tamthilia teule. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili vipengele vya muundo na mtindo wa tamthilia teule akiwa na wenzake.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kupata vipengele vya muundo na mtindo. Pia anapotazama mchezo wa kuigiza kwenye mtandao wa *You Tube*.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni ili kupata vipengele vya muundo na mtindo.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapofanya utafiti kwa kusakura mtandao salama ili kupata vipengele vya muundo na mtindo.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya muundo na mtindo katika tamthilia teule.
- Heshima: mwanafunzi anapotathmini kazi iliyowasilishwa na wenzake darasani kuhusu vipengele vya muundo na mtindo huku akithamini maoni wa kila mmoja.

**Masuala Mtambuko:**

Kujiamini: mwanafunzi anapowawasilishia wenzake kwa ujasiri matokeo ya utafiti wake kuhusu vipengele vya muundo na mtindo.

DRAFT

| 5.0 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **5.1 Fasihi Simulizi** | **5.1.1 Mazungumzo** (Vipindi 8) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza dhana ya mazungumzo katika fasihi simulizi ili kuibanisha,<br>b) kufafanua sifa za mazungumzo katika fasihi simulizi,<br>c) kujadili dhima ya mazungumzo katika fasihi simulizi,<br>d) kujadili sifa za mazungumzo katika matini ya fasihi simulizi,<br>e) kupambanua miktadha mbalimbali ya mazungumzo katika fasihi simulizi, | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza dhana ya mazungumzo katika fasihi simulizi,<br>• kutaja vipera mbalimbali vya utanzu wa mazungumzo ya fasihi simulizi,<br>• kusikiliza matini za mazungumzo ya fasihi simulizi katika vifaa vya kidijitali,<br>• kufafanua sifa za mazungumzo kutoka kwenye matini alizosikiliza,<br>• kujadili na wenzake sifa za mazungumzo katika matini ya fasihi simulizi,<br>• kuigiza baadhi ya vipera vya mazungumzo, | Kuna aina gani za mazungumzo ya fasihi simulizi? |

DRAFT

<table>
<tr><td></td><td></td><td>f) kuchangamkia mazungumzo katika fasihi simulizi.</td><td>• kujadili na wenzake umuhimu wa mazungumzo katika fasihi simulizi.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili vipera mbalimbali vya mazungumzo akiwa na wenzake.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anaposikiliza matini mbalimbali yanayohusu mazungumzo kwenye vifaa vya kidijitali.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapojadiliana kuhusu mazungumzo katika fasihi simulizi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji akiwa darasani.<br>• Uwajibikaji anaposikiliza matini mbalimbali kwenye vifaa vya kidijitali.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala Mtambuko:<br>Stadi za maisha anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.</td></tr>
</table>

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.2 Ushairi** | **5.2.1 Uchambuzi wa Mandhari na Wahusika** (Vipindi 6) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya mandhari na wahusika katika ushairi,<br>b) kujadili aina za mandhari na wahusika katika ushairi,<br>c) kujadili umuhimu wa mandhari katika ushairi,<br>d) kuchambua mandhari na wahusika katika ushairi,<br>e) kuchangamkia mandhari na wahusika katika ushairi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya mandhari na wahusika katika mashairi,<br>• kujadili aina za mandhari katika mashairi,<br>• kujadili aina za wahusika *(nafsineni na nafsinenewa)* katika mashairi,<br>• kuchambua mandhari na wahusika katika matini za ushairi,<br>• kuwasilisha uchambuzi wa mandhari na wahusika katika ushairi,<br>• kutafiti vitabuni na mtandaoni kuhusu wahusika na mandhari,<br>• kuwasilisha matokeo ya utafiti kwa wenzake ili wautathmini. | Mandhari yana umuhimu gani katika shairi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Kujiamini: mwanafunzi anapowasilisha uchambuzi wa mandhari na wahusika katika ushairi.
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili na wenzake umuhimu wa mandhari.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochambua mandhari na wahusika katika mashairi.

DRAFT

| |
|---|
| • Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotafiti mitandaoni kuhusu wahusika na mandhari. |
| **Maadili:**<br>• Umoja- mwanafunzi anapohusiana vizuri na wenzake vyema wakati wa kuchambua wahusika na mandhari.<br>• Uwajibikaji - mwanafunzi anapochambua wahusika na mandhari katika mashairi na kutunza kifaa cha kidijitali.<br>• Heshima - mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu wahusika na mandhari. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala mtambuko anuwai katika mashairi mbalimbali. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.3 Bunilizi** | **5.3.1 Tamthilia**<br>- *Muundo*<br>- *Mtindo*<br><br>(Vipindi 12) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya muundo na mtindo katika tamthilia,<br>b) kujadili vipengele vya muundo na mtindo katika tamthilia teule,<br>c) kutathmini nafasi ya vipengele vya muundo na mtindo katika tamthilia teule,<br>d) kuchambua tamthilia teule kwa kuzingatia muundo na mtindo wake,<br>e) kuonea fahari muundo na mtindo katika tamthilia. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusoma tamthilia teule na kutambua vipengele vya muundo na mtindo,<br>• kujadili na wenzake vipengele vya muundo na mtindo katika tamthilia teule,<br>• kuwasilisha darasani vipengele vya muundo na mtindo ili wenzake wavitathmini,<br>• kutazama mchezo unaoigizwa kwenye video na kujadili vipengele vya muundo na mtindo,<br>• kuigiza sehemu ya tamthilia ili kubainisha vipengele vya muundo na mtindo. | Kuna tofauti gani kati ya muundo na mtindo wa tamthilia? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili vipengele vya muundo na mtindo wa tamthilia teule akiwa na wenzake.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoigiza sehemu ya mchezo ili kubainisha muundo na mtindo.

| |
|---|
| • Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni ili kupata vipengele vya muundo na mtindo. |
| **Maadili:**<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapofanya utafiti kwa kusakura mtandao salama ili kupata vipengele vya muundo na mtindo.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake vipengele vya muundo na mtindo katika tamthilia teule.<br>• Heshima: mwanafunzi anapotathmini kazi iliyowasilishwa na wenzake darasani kuhusu vipengele vya muundo na mtindo huku akithamini maoni wa kila mmoja. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Kujiamini: mwanafunzi anapowawasilishia wenzake kwa ujasiri matokeo ya utafiti wake kuhusu vipengele vya muundo na mtindo. |

DRAFT

<table>
<tr><td colspan="5">6.0</td></tr>
<tr><th>Mada</th><th>Mada Ndogo</th><th>Matokeo Maalum Yanayotarajiwa</th><th>Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa</th><th>Swali Dadisi Lililopendekezwa</th></tr>
<tr><td>6.1 Fasihi Simulizi</td><td>6.1.1 Maigizo<br><br>(Vipindi 6)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza dhana ya maigizo ili kuibanisha,<br>b) kufafanua sifa za maigizo ili kuzibainisha,<br>c) kujadili umuhimu wa maigizo katika jamii,<br>d) kuigiza vipera vya maigizo ya fasihi simulizi,<br>e) kuchangamkia umuhimu wa maigizo katika jamii yake.</td><td>Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza dhana ya maigizo katika fasihi simulizi,<br>• kutazama maigizo kwenye kifaa cha kidijitali,<br>• kufafanua sifa za maigizo kutoka kwenye maigizo aliyotazama,<br>• kujadili na wenzake dhima ya maigizo,<br>• kuchambua maigizo kwa kuzingatia sifa zake,<br>• kujadili vipera mbalimbali vya maigizo katika fasihi simulizi,<br>• kurekodi maigizo katika kifaa cha kidijitali.</td><td>Maigizo ya fasihi simulizi yana umuhimu gani?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano:mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadiliana kuhusu maigizo.<br>• Ujuzi wa kidijitali : mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kurekodi maigizo.<br>• Uraia: mwanafunzi anapojiunza kuhusu umuhimu wa maigizo katika fasihi simulizi.</td></tr>
</table>

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Umoja:mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Heshima:mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapojadiliana kuhusu maigizo.<br>• Uwajibikaji:mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali wanaporekodi maigizo.<br>• Uadilifu: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kurekodi maigizo. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Stadi za maisha: mwanafunzi anapojadili mifano ya mazungumzo. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.2 Ushairi** | **6.2.1 Uchambuzi wa Muundo**<br><br>(Vipindi 5) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya muundo ili kuupambanua,<br>b) kujadili vipengele vya muundo katika mashairi,<br>c) kufafanua umuhimu wa vipengele vya muundo katika shairi,<br>d) kuchambua mashairi kwa kuzingatia vipengele vya muundo,<br>e) kufurahia kuchambua mashairi kwa kuzingatia vipengele vyake. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya muundo,<br>• kujadili vipengele vya muundo katika mashairi,<br>• kuchambua muundo katika mashairi vitabuni au mitandaoni,<br>• kufafanua umuhimu wa vipengele vya muundo katika mashairi mbalimbali,<br>• kutazama video zilizorekodiwa za uchambuzi wa kitaalamu wa mashairi<br>• kuwarekodi wenzake wakiwasilisha uchambuzi wa mashairi darasani kwa hifadhi ya marejeleo. | Vipengele vya muundo vina umuhimu gani katika shairi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili na wenzake kuhusu muundo wa mashairi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochambua muundo wa mashairi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapochambua muundo mashairi mitandaoni na kurekodi mawasilisho ya wenzake akitumia vyombo vya kidijitali.

| |
|---|
| • Kujiamini: mwanafunzi anapowasilisha uchambuzi wa muundo wa mashairi. |
| **Maadili:**<br>• Umoja- mwanafunzi anapohusiana vizuri na wenzake wakati wa kuchambua muundo wa mashairi.<br>• Uwajibikaji - mwanafunzi anapochambua muundo wa mashairi mitandaoni na kutunza kifaa cha kidijitali.<br>• Heshima - mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu muundo wa mashairi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala mtambuko anuwai katika mashairi mbalimbali. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **6.3 Bunilizi** | **6.3.1 Riwaya**<br>- *Maudhui*<br>- *Dhamira*<br><br>(Vipindi 10) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya maudhui na dhamira katika riwaya teule,<br>b) kutambua maudhui na dhamira katika riwaya teule,<br>c) kueleza namna maudhui yanavyowasilishwa katika riwaya,<br>d) kuchanganua maudhui na dhamira katika riwaya teule,<br>e) kuchangamkia maudhui na dhamira katika riwaya. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusakura mtandaoni maana ya maudhui na dhamira katika riwaya akiwa na wenzake,<br>• kusoma riwaya teule na kuchambua maudhui na dhamira,<br>• kueleza namna maudhui yanavyowasilishwa katika riwaya,<br>• kuandika maelezo kuhusu maudhui na dhamira katika riwaya aliyosoma na kuyawasilisha kwa wenzake ili wayatathmini. | Je, riwaya huweza kuzungumzia mambo gani? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapochanganua maudhui na dhamira katika riwaya teule akiwa na wenzake.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kupata maana ya maudhui na dhamira.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua maneno maalum yanayotofautisha maudhui na dhamira.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni ili kupata maana ya dhamira na maudhui.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanapochanganua maudhui na dhamira katika riwaya teule.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya kazi ya kikundi |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala mtambuko anuwai kutegemea maudhui katika riwaya teule (*k.v. kujiamini, uhifadhi wa mazingira, upatanisho, utangamano wa kijamii*). |

DRAFT

| 7.0 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Maswali dadisi Yaliyopendekezwa** |
| **7.1 Fasihi Simulizi** | **7.1.1 Hadithi**<br>- *Ngano za mazimwi*<br>- *Mighani*<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya ngano za mazimwi na mighani,<br>b) kufafanua sifa za ngano za mazimwi na mighani,<br>c) kujadili vipengele vya ngano za mazimwi na mighani,<br>d) kujadili umuhimu wa ngano za mazimwi na mighani katika jamii,<br>e) kuchanganua ngano za mazimwi na mighani kwa kuzingatia vipengele vyake,<br>f) kufurahia masimulizi ya ngano za mazimwi na mighani kutoka jamii mbalimbali. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya ngano za mazimwi na mighani,<br>• kusikiliza masimulizi yaliyorekodiwa kwenye kifaa cha kidijitali kuhusu ngano za mazimwi na mighani,<br>• kufafanua sifa za ngano za mazimwi na mighani,<br>• kusakura mtandaoni kuhusu umuhimu wa ngano za mazimwi na mighani katika jamii,<br>• kutafiti kuhusu ngano za mazimwi na mighani kutoka kwa jamii,<br>• kuwasilisha matokeo ya utafiti wake kwa wenzake ili wayatathmini,<br>• kufanya kazi mradi kuhusu ngano za mazimwi au mighani. | 1. Je, ngano zina umuhimu gani katika jamii yako?<br>2. Ni mambo gani unayoweza kujifunza kutokana na ngano za mazimwi katika jamii ya sasa? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa ngano za *mazimwi* au *mighani* katika jamii.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapofanya kazi mradi kuhusu ngano za mazimwi au mighani.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapofanya kazi mradi kuhusu ngano za *mazimwi* au *mighani*.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofanya kazi mradi kuhusu ngano za *mazimwi* au *mighani*.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapofanya kazi mradi kuhusu ngano za *mazimwi* au *mighani*.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa ngano za *mazimwi* au *mighani* katika jamii. |
| **Maadili**<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapofanya kazi mradi kuhusu ngano za mazimwi au mighani.<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanajadiliana kuhusu umuhimu wa ngano za mazimwi na mighani katika jamii.<br>• Umoja: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanajadiliana kuhusu umuhimu wa ngano za mazimwi na mighani katika jamii.<br>• Uadilifu: mwanafunzi anapofanya kazi mradi kuhusu ngano za *mazimwi* au *mighani*. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusakura maeneo salama kuhusu umuhimu wa ngano za mazimwi na mighani katika jamii.<br>• Uraia: mwanafunzi anaposimulia ngano za mazimwi na mighani kutoka jamii mbalimbali.<br>• Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposimulia ngano za mazimwi na mighani kutoka jamii mbalimbali.<br>• Utambuzi wa tamaduni mbalimbali: mwanafunzi anaposimulia ngano za mazimwi na mighani kutoka jamii mbalimbali. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.2 Ushairi** | **7.2.1 Mtindo -**<br>- *Tashbihi*<br>- *Sitiari*<br>- *Tashihisi*<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya tashbihi, sitiari na tashihisi kama vipengele vya kimtindo,<br>b) kutambua tashbihi, sitiari na tashihisi katika ushairi,<br>c) kujadili umuhimu wa tashbihi, sitiari na tashihisi katika ushairi,<br>d) kutathmini nafasi ya tashbihi, sitiari na tashihisi katika mashairi,<br>e) kufurahia matumizi ya tashbihi, sitiari na tashihisi katika mashairi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya tashbihi, sitiari na tashihisi kama vipengele vya kimtindo,<br>• kutambua tashbihi, sitiari na tashihisi katika matini za kishairi,<br>• kutafiti mtandaoni au katika matini andishi kuhusu umuhimu wa tashbihi, sitiari na tashihisi katika ushairi,<br>• kujadili matumizi ya tashbihi, sitiari na tashihisi katika mashairi na kuwawasilishia wenzake ili wayatathmini. | Tamathali za usemi zina umuhimu gani katika ushairi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapochambua matumizi ya tashbihi, sitiari na tashihisi na wenzake darasani.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotafiti kuhusu tashibihi, sitiari na tashihisi mitandaoni.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua na anapochambua tashbihi,sitiari na tashihisi katika mashairi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni ili kupata umuhimu wa tashbihi, sitiari na tashihisi.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Umoja- mwanafunzi anapohusiana vizuri na wenzake wakati wa kuchambua tashbihi, sitiari na tashihisi.<br>• Uwajibikaji - mwanafunzi anapochambua tashbihi, sitiari na tashihisi katika mashairi na kutunza kifaa cha kidijitali.<br>• Heshima - mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu tashbihi, sitiari na tashihisi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala mtambuko mbalimbali katika mashairi atakayosoma. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.3 Bunilizi** | **7.3.1 Riwaya**<br>- *Wahusika*<br>- *Mandhari*<br><br>(Vipindi 10) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza dhana ya wahusika na mandhari katika riwaya,<br>b) kujadili usawiri wa wahusika katika riwaya teule,<br>c) kueleza umuhimu wa wahusika katika riwaya,<br>d) kueleza umuhimu wa mandhari katika riwaya,<br>e) kujadili aina za mandhari katika riwaya,<br>f) kuchangamkia wahusika na mandhari katika riwaya. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua wahusika katika riwaya teule,<br>● kujadili usawiri wa wahusika katika riwaya teule,<br>● kujadili mafunzo yanayotokana na matendo ya wahusika katika riwaya,<br>● kuchanganua umuhimu wa wahusika katika riwaya teule,<br>● kueleza dhana ya mandhari katika riwaya kwa kuzingatia mahali pa tukio, wakati na hali,<br>● kujadili aina za mandhari katika riwaya,<br>● kuchambua mandhari katika riwaya teule na kujadili na wenzake mahali, hali na wakati wa matukio.<br>● kutafiti mtandaoni au katika matini andishi maelezo kuhusu mandhari na wahusika na kujadili na wenzake, | 1. Mahali na wakati unaorejelewa katika riwaya huwa na umuhimu gani?<br>2. Usawiri wa wahusika una umuhimu gani katika riwaya? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● kutathmini maelezo ya wenzake kuhusu mandhari na wahusika. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano: mwanafunzi anapoeleza wenzake kwa ufasaha kuhusu dhana ya mandhari katika riwaya.
- Ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuchambua mandhari katika riwaya teule.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni au katika matini andishi maelezo kuhusu mandhari na wahusika.
- Kujiamini: mwanafunzi anapojadili na wenzake na kuchangia kikamilifu maelezo kuhusu mandhari na kutathmini maelezo yao.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni na kusoma maelezo kuhusu mandhari na wahusika katika riwaya.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuchambua mandhari katika riwaya teule.
- Heshima: mwanafunzi anapotathmini maelezo ya wenzake kuhusu mandhari na wahusika huku akithamini mchango wa kila mmoja.

**Masuala Mtambuko:**

Kujiamini**:** mwanafunzi anapowasilisha maoni yake kuhusu wahusika na mandhari kwa wenzake kwa ujasiri.

DRAFT

| **8.0** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **8.1 Fasihi Simulizi** | **8.1.1 Semi**<br>- *Misemo*<br>- *Nahau*<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya misemo na nahau ili kuipambanua,<br>b) kutambua misemo na nahau katika matini ya fasihi simulizi,<br>c) kujadili vipengele vya misemo na nahau mbalimbali,<br>d) kuchanganua misemo na nahau katika matini,<br>e) kujadili nafasi ya misemo na nahau katika jamii,<br>f) kutumia misemo na nahau katika tungo za fasihi simulizi,<br>g) kuchangamkia matumizi ya misemo na nahau katika tungo za fasihi simulizi | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya misemo na nahau,<br>● kutambua misemo na nahau kutoka kwenye tungo simulizi au kifaa cha kidijitali,<br>● kujadili vipengele vya misemo na nahau mbalimbali,<br>● kutumia kifaa cha kidijitali kusakura matumizi ya misemo na nahau katika tungo za fasihi simulizi,<br>● kujadili nafasi ya misemo na nahau katika jamii,<br>● kujadili kwa kushirikiana na wenzake matumizi ya misemo na nahau,<br>● kuwasilisha misemo na nahau katika jamii. | Misemo na nahau zina umuhimu gani katika jamii? |

DRAFT

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili matumizi ya misemo na nahau.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusakura kuhusu misemo na nahau.<br>● Uraia: mwanafunzi anapojifunza misemo na nahau katika jamii yake. |
| **Maadili:**<br>● Uzalendo: mwanafunzi anapoeleza matumizi ya misemo na nahau katika jamii yake.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi katika shughuli ya ujifunzaji.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia darasani. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapozingatia usalama wake anaposakura mtandaoni kuhusu misemo na nahau. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.2 Ushairi** | **8.2.1 Mtindo**<br>- *Misemo*<br>- *Nahau*<br>- *Chuku*<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya misemo, nahau na chuku kama vipengele vya kimtindo,<br>b) kutambua misemo, nahau na chuku katika matini za kishairi,<br>c) kueleza umuhimu wa misemo, nahau na chuku katika ushairi,<br>d) kutathmini nafasi ya misemo, nahau na chuku katika ushairi,<br>e) kufurahia matumizi ya misemo, nahau na chuku katika ushairi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya misemo, nahau na chuku kama vipengele vya kimtindo,<br>● kutambua misemo, nahau na chuku katika matini za kishairi,<br>● kutafiti mtandaoni au matini andishi umuhimu wa misemo, nahau na chuku katika ushairi,<br>● kutathmini nafasi ya misemo, nahau na chuku katika ushairi,<br>● kuchambua matumizi ya misemo, nahau na chuku katika mashairi na kuwawasilishia wenzake ili wayatathmini. | Tamathali za usemi zina nafasi gani katika ushairi? |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapochambua matumizi ya misemo, nahau na chuku na wenzake darasani.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotafiti kuhusu misemo, nahau na chuku mitandaoni. | | | | |

| |
|---|
| ● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua na anapochambua misemo, nahau na chuku katika mashairi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni ili kupata umuhimu wa misemo, nahau na chuku.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapowasilisha darasani uchambuzi wa matumizi ya misemo, nahau, na chuku. |
| **Maadili:**<br>● Umoja- mwanafunzi anapohusiana vizuri na wenzake wakati wa kuchambua misemo, nahau na chuku.<br>● Uwajibikaji - mwanafunzi anapochambua misemo, nahau na chuku katika mashairi na kutunza kifaa cha kidijitali.<br>● Heshima - mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu misemo, nahau na chuku. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala mtambuko mbalimbali katika mashairi atakayosoma. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.3 Bunilizi** | **8.3.1 Riwaya**<br>- *Muundo*<br>- *Mtindo*<br><br>(Vipindi 8) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya muundo na mtindo katika riwaya,<br>b) kujadili vipengele vya muundo na mtindo katika fasihi,<br>c) kuchanganua muundo na mtindo katika riwaya,<br>d) kuchangamkia muundo na mtindo katika riwaya. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya muundo na mtindo katika riwaya,<br>● kujadili vipengele vya muundo katika riwaya teule darasani akiwa na wenzake,<br>● kufanya utafiti mtandaoni na katika matini andishi kuhusu vipengele vya muundo na mtindo na kuwawasilishia wenzake ili watathmini matokeo yake,<br>● kuandaa uchanganuzi wa muundo na mtindo wa riwaya teule na kuwawasilishia wenzake ili wautolee maoni. | Je, waandishi wa riwaya huyapangaje mawazo yao ili kuwasilisha ujumbe? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili vipengele vya muundo na mtindo wa riwaya teule akiwa na wenzake.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kupata vipengele vya muundo na mtindo wa riwaya.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni ili kupata vipengele vya muundo na mtindo.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapofanya utafiti kwa kusakura mtandao salama ili kupata vipengele vya muundo na mtindo.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya muundo na mtindo katika riwaya teule.<br>● Heshima: mwanafunzi anapotathmini kazi iliyowasilishwa na wenzake darasani kuhusu vipengele vya muundo na mtindo huku akithamini maoni wa kila mmoja. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Kujiamini: mwanafunzi anapowawasilishia wenzake kwa ujasiri matokeo ya utafiti wake kuhusu vipengele vya muundo na mtindo. |

DRAFT

| 9.0 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **9.1 Fasihi Simulizi** | **9.1.1 Ushairi simulizi**<br><br>*Nyimbo*<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya nyimbo kama kipera cha ushairi simulizi,<br>b) kujadili aina mbalimbali za nyimbo katika fasihi simulizi ili kuzitofautisha,<br>c) kufafanua sifa za nyimbo katika ushairi simulizi,<br>d) kujadili dhima za nyimbo katika jamii,<br>e) kuchanganua nyimbo kwa kuzingatia sifa zake,<br>f) kufurahia nyimbo za aina mbalimbali kutoka jamii tofauti tofauti. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya nyimbo kama kipera cha ushairi simulizi,<br>● kusikiliza nyimbo zilizorekodiwa katika kifaa cha kidijitali ili kufafanua sifa zake,<br>● kutambua aina mbalimbali za nyimbo alizosikiliza katika kifaa cha kidijitali,<br>● kutumia kifaa cha kidijitali kusakura mtandaoni kuhusu dhima ya nyimbo katika jamii,<br>● kufanya utafiti kuhusu aina mbalimbali za nyimbo katika jamii na kuwasilisha matokeo ya utafiti wake kwa wenzake ili wayatathmini,<br>● kuchanganua aina mbalimbali za nyimbo alizopata kutoka jamii yake, | Je, nyimbo zina umuhimu gani katika jamii? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● kuwaimbia wenzake nyimbo za aina mbalimbali. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili dhima za nyimbo katika jamii.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochanganua aina mbali mbali za nyimbo kutoka jamii yake.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga na kuimba nyimbo za aina mbalimbali kutoka jamii yake.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusakura mtandaoni kuhusu dhima za nyimbo katika jamii.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofanya utafiti kuhusu aina mbali mbali za nyimbo kutoka jamii yake.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasilisha matokeo ya utafiti wake kwa wenzake ili wayatathmini.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anaposakura maeneo salama mtandaoni anapotafiti kuhusu dhima za nyimbo katika jamii yake.
- Heshima: anapoyathamini maoni ya wenzake anapowasilisha matokeo ya utafiti wake.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili dhima ya nyimbo katika jamii.
- Uadilifu: mwanafunzi anapozingatia maadili anapofanya utafiti wake.

**Masuala Mtambuko:**

- Uraia: mwanafunzi anapotunga na kuimba nyimbo kutoka jamii tofautitofauti.
- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapotunga na kuimba nyimbo kutoka jamii tofautitofauti.
- Usalama mtandaoni: mwanafunzi anaposakura maeneo salama mtandaoni anapotafiti kuhusu dhima za nyimbo katika jamii yake.
- Utambuzi wa tamaduni mbalimbali: mwanafunzi anapotunga na kuimba nyimbo kutoka jamii tofautitofauti.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.2 Ushairi** | **9.2.1 Uhuru wa Kishairi**<br><br>- *Inkisari*<br>- *Mazida*<br>- *Tabdila*<br>- *kuboronga sarufi*<br><br>(Vipindi 5)<br><br>- | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya uhuru wa kishairi ili kuipambanua,<br>b) kueleza maana ya inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi kama vipengele vya uhuru wa kishairi,<br>c) kutambua matumizi ya inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi katika mashairi,<br>d) kujadili umuhimu wa inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi katika mashairi,<br>e) kufurahia matumizi ya inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi katika mashairi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya uhuru wa kishairi,<br>● kueleza maana ya inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi kama vipengele vya uhuru wa kishairi,<br>● kutambua matumizi ya inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi katika mashairi,<br>● kujadili umuhimu wa inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi katika mashairi,<br>● kutafiti mtandaoni au katika matini andishi kuhusu umuhimu wa inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi,<br>● kuwawasilishia wenzake tathmini yake kuhusu inkisari, mazida, tabdila na | 1. Uhuru wa kishairi unahusu nini?<br>2. Uhuru wa kishairi una nafasi gani katika utunzi wa mashairi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuboronga sarufi katika mashairi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi katika ushairi
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusakura mtandaoni umuhimu ya inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofanya utafiti kuhusu matumizi ya inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotathmini matumizi ya inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anapohusiana vizuri na wenzake wakati wa kuchambua matumizi ya inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapochambua matumizi ya inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi katika mashairi na kutunza kifaa cha kidijitali.
- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu matumizi ya inkisari, mazida, tabdila na kuboronga sarufi katika mashairi.

**Masuala Mtambuko:**

Masuala anuwai katika mashairi mbalimbali atakayosoma.

DRAFT

<table>
<tr><th>Mada</th><th>Mada Ndogo</th><th>Matokeo Maalum Yanayotarajiwa</th><th>Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa</th><th>Swali Dadisi Lililopendekezwa</th></tr>
<tr><td>9.3 Bunilizi</td><td>9.3.1 Riwaya<br>- Muundo<br>- Mtindo<br><br>(Vipindi 8)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya muundo na mtindo katika riwaya teule,<br>b) kuchanganua vipengele vya muundo na mtindo katika riwaya teule,<br>c) kuchangamkia uchanganuzi wa muundo na mtindo katika riwaya.</td><td>Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vipengele vya muundo na mtindo katika riwaya teule,<br>• kusoma riwaya teule na kutambua vipengele vya muundo na mtindo,<br>• kujadili na wenzake vipengele vya muundo na mtindo katika riwaya teule,<br>• kusakura mtandaoni kutazama video au kusoma matini andishi kuhusu vipengele vya muundo na mtindo katika riwaya,<br>• kuwasilisha vipengele vya muundo na mtindo ili wenzake wavitathmini.</td><td>Waandishi wa riwaya huwezaje kuzifanya kazi zao kuwa za kuvutia kwa wasomaji?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili vipengele vya muundo na mtindo wa riwaya teule akiwa na wenzake.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapojadili na wenzake kuhusu muundo na mtindo katika riwaya teule<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni ili kupata vipengele vya muundo na mtindo.</td></tr>
</table>

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapofanya utafiti kwa kusakura mitandaoni ili kupata vipengele vya muundo na mtindo.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya muundo na mtindo katika riwaya teule.<br>• Heshima: mwanafunzi anapotathmini kazi iliyowasilishwa na wenzake darasani kuhusu vipengele vya muundo na mtindo. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Kujiamini: mwanafunzi anapowawasilishia wenzake kwa ujasiri matokeo ya utafiti wake kuhusu vipengele vya muundo na mtindo. |

DRAFT

| 10.0 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **10.1 Fasihi Simulizi** | **10.1.1 Ushairi Simulizi**<br>- *Maghani ya kawaida*<br><br>(Vipindi 6) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya maghani ya kawaida kama kipera cha ushairi simulizi,<br>b) kueleza maana ya majigambo, pembezi na tondozi kama aina za maghani ya kawaida,<br>c) kueleza sifa za majigambo, pembezi na tondozi kama aina za maghani ya kawaida,<br>d) kujadili umuhimu wa majigambo, pembezi na tondozi katika jamii,<br>e) kueleza vipengele vya majigambo, pembezi na tondozi kama aina za maghani ya kawaida, | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya maghani ya kawaida kama kipera cha ushairi simulizi,<br>● kusakura mtandaoni au kutafiti katika matini andishi kuhusu sifa za majigambo, pembezi na tondozi,<br>● kuwasilisha matokeo ya utafiti wake kwa wenzake ili wayatolee maoni,<br>● kushirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa majigambo, pembezi na tondozi katika jamii,<br>● kutafiti kuhusu majigambo, pembezi na tondozi katika jamii yake na kuwasilisha matokeo ya utafiti wake, | Je, unafahamu nini kuhusu majigambo, pembezi na tondozi? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | f) kuchanganua vipengele vya majigambo, pembezi na tondozi katika matini,<br>g) kufurahia matumizi ya majigambo, pembezi na tondozi katika miktadha mbalimbali ya kijamii. | ● kuwawasilishia wenzake majigambo, pembezi au tondozi,<br>● kueleza vipengele vya majigambo, pembezi na tondozi kama aina za maghani ya kawaida,<br>● kuchanganua vipengele vya majigambo, pembezi na tondozi katika matini,<br>● kuwasilisha ripoti ya utafiti wake kwa wenzake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzke kujadili umuhimu wa majigambo, pembezi na tondozi katika jamii.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusakura mtandaoni sifa za majigambo, pembezi na tondozi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofanya utafiti kuhusu matumizi ya majigambo, pembezi na tondozi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapoadika ripoti ya utafiti wake.
- Ubunifu: mwanafunzi anapowasilisha ripoti ya utafiti kuhusu matumizi ya majigambo, pembezi na tondozi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapojadiliana kuhusu umuhimu wa majigambo,pembezi na tondozi katika jamii.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa majigambo, pembezi na tondozi katika jamii.

| |
|---|
| ● Uwajibikaji: mwanafunzi anaposhiriki katika utafiti kuhusu matumizi ya majigambo, pembezi na tondozi katika jamii yake.<br>● Uadilifu: mwanafunzi anapofanya utafiti kuhusu matumizi ya majigambo, pembezi na tondozi katika jamii yake.<br>● Amani: mwanafunzi anapotangamana na watu katika jamii yake anapofanya utafiti kuhusu matumizi ya majigambo, pembezi na tondozi katika jamii yake. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapofanya utafiti kuhusu matumizi ya majigambo, pembezi na tondozi katika jamii yake.<br>● Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotumia mtandao salama katika utafiti kuhusu matumizi ya majigambo, pembezi na tondozi katika jamii yake.<br>● Uraia: mwanafunzi anapofanya utafiti kuhusu matumizi ya majigambo, pembezi na tondozi katika jamii yake. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Ushairi** | **10.2.1 Uhuru wa Kishairi**<br>- *Matumizi ya Lahaja*<br>- *Utohozi*<br>- *Lugha ya Kale*<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya lahaja, utohozi na lugha ya kale kama vipengele vya uhuru wa kishairi,<br>b) kutambua matumizi ya lahaja, utohozi na lugha ya kale katika mashairi,<br>c) kujadili umuhimu wa lahaja, utohozi na lugha ya kale katika mashairi,<br>d) kuchambua mashairi kwa kuzingatia matumizi ya lahaja, utohozi na lugha ya kale,<br>e) kufurahia matumizi ya lahaja, utohozi na lugha ya kale katika mashairi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya lahaja, utohozi na lugha ya kale kama vipengele vya uhuru wa kishairi,<br>● kutambua matumizi ya lahaja, utohozi na lugha ya kale katika mashairi,<br>● kutafiti mtandaoni au matini andishi matumizi ya lahaja, utohozi na lugha ya kale katika mashairi,<br>● kujadili umuhimu wa lahaja, utohozi na lugha ya kale katika mashairi,<br>● kuchambua mashairi ili kuonyesha matumizi wa lahaja, utohozi na lugha ya kale. | Lahaja, utohozi na lugha ya kale humsaidiaje mtunzi wa shairi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa lahaja, utohozi na lugha ya kale katika ushairi<br>● Ujuzi wa kidijitali : mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusakura mtandaoni matumizi ya lahaja, utohozi na lugha ya kale katika mashairi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofanya utafiti kuhusu matumizi ya lahaja, utohozi na lugha ya kale katika mashairi.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotathmini matumizi ya lahaja, utohozi na lugha ya kale katika mashairi. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anapohusiana vizuri na wenzake wakati wa kuchambua matumizi ya lahaja, utohozi na lugha ya kale katika mashairi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapochambua matumizi ya lahaja, utohozi na lugha ya kale katika mashairi na kutunza kifaa cha kidijitali.<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake kuhusu matumizi ya lahaja, utohozi na lugha ya kale katika mashairi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala anuwai katika mashairi mbalimbali atakayosoma. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.3 Bunilizi** | **10.3.1** *Utunzi wa mashairi na bunilizi*<br><br>(Vipindi 4) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya utunzi wa mashairi na bunilizi ili kuvibainisha,<br>b) kupambanua hatua za utunzi wa mashairi na bunilizi ili kuzitambulisha,<br>c) kuandika shairi au bunilizi fupi kwa kuzingatia vipengele na hatua za utunzi wa kazi ya fasihi,<br>d) kuonea fahari utunzi wa bunilizi katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vipengele na hatua za utunzi wa mashairi na bunilizi,<br>● kutafiti katika matini andishi au mtandaoni ili kutambua vipengele vya utunzi wa mashairi na bunilizi,<br>● kuwawasilishia wenzake vipengele na hatua za utunzi wa mashairi na bunilizi alivyotafiti ili wavitathmini,<br>● kuandika shairi au bunilizi fupi kwa kuzingatia vipengele na hatua za utunzi zifaazo,<br>● kusoma shairi au bunilizi fupi aliyotunga ili wenzake waitolee maoni. | Utunzi wa bunilizi una manufaa gani maishani? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowasilisha matokeo ya utafiti wake kuhusu vipengele vya uandishi kwa wenzake ili wayatolee maoni.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowawasilishia wenzake kwa ufasaha matokeo ya utafiti wake ili wayatolee maoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika aya fupi fupi za makala mbalimbali kwa kuzingatia hatua zifaazo.

DRAFT

| |
|---|
| ● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti maktabani na mtandaoni iili kubainisha vipengele na hatua za uandishi wa fasihi bunilizi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi kutafiti anaposakura mtandaoni ili kubainisha aina za fasihi bunilizi. |
| **Maadili:**<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapofanya utafiti kwa kusakura mtandao kuhusu hatua za uandishi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya uandishi bunilizi.<br>● Heshima: mwanafunzi anapotathmini kazi iliyowasilishwa na wenzake darasani kuhusu vipengele na hatua za uandishi bunifu huku akithamini maoni wa kila mmoja. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Kujiamini: mwanafunzi anapowawasilishia wenzake kwa ujasiri matokeo ya utafiti wake kuhusu vipengele na hatua za uandishi bunilizi. |

DRAFT

## VIGEZO NA VIWANGO VYA KUZINGATIA KATIKA KUTATHMINI

### Fasihi Simulizi

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuweza kuchambua hadithi za fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake. | Anachambua kwa kina hadithi za fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake kwa utondoti. | Anachambua hadithi za fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake. | Anachambua hadithi za fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake. | Anachambua hadithi za fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake kwa kuelekezwa. |
| Kuweza kuchanganua semi za fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake. | Anachanganua kwa kina semi za fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake. | Anachanganua semi za fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake. | Anachanganua semi za fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake. | Anachanganua semi za fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake kwa kusaidiwa. |
| Kuweza kuchambua maigizo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake. | Anachambua maigizo ya fasihi simulizi kwa uketo kwa kuzingatia vipengele vyake. | Anachambua maigizo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake. | Anachambua maigizo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake. | Anachambua maigizo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake kwa kuongozwa. |

DRAFT

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuweza kuchanganua mashairi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake. | Anachanganua mashairi simulizi kwa utondoti kwa kuzingatia vipengele vyake. | Anachanganua mashairi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake. | Anachanganua mashairi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake. | Anachanganua mashairi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake kwa kusaidiwa. |
| Kuweza kuchambua mazungumzo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake. | Anachambua kwa kina mazungumzo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake. | Anachambua mazungumzo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia vipengele vyake. | Anachambua mazungumzo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake. | Anachambua mazungumzo ya fasihi simulizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vyake kwa kusaidiwa. |

**Ushairi**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuweza kuainisha mashairi kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya uainishaji. | Anaainisha mashairi kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya uainishaji kwa utondoti. | Anaainisha mashairi kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya uainishaji. | Anaainisha mashairi kwa kuzingatia baadhi ya vigezo vya uainishaji. | Anaainisha mashairi kwa kuzingatia baaadhi ya vigezo vya uainishaji kwa kuelekezwa. |
| Kuweza kuchambua mashairi kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya ushairi. | Anachambua kwa kina mashairi kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya ushairi. | Anachambua mashairi kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya ushairi. | Anachambua mashairi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya ushairi. | Anachambua mashairi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya ushairi kwa kusaidiwa. |

DRAFT

**Bunilizi**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuweza kuchambua vipengele vyote vya bunilizi. | Anachambua kwa utondoti vipengele vyote vya bunilizi. | Anachambua vipengele vyote vya bunilizi. | Anachambua baadhi ya vipengele vya bunilizi. | Anachambua baadhi ya vipengele vya bunilizi kwa kuelekezwa. |
| Kuweza kutunga bunilizi kwa kuzingatia vipengele na hatua zifaazo. | Anatunga bunilizi ya kiwango cha juu cha ubunifu kwa kuzingatia vipengele na hatua zifaazo. | Anatunga bunilizi kwa kuzingatia vipengele na hatua zifaazo. | Anatunga bunilizi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele na hatua zifaazo. | Anaelekezwa kutunga bunilizi kwa kuzingatia vipengele na hatua zifaazo. |

DRAFT

JAMHURI YA KENYA
WIZARA YA ELIMU
Mali ya serikali ya Kenya
HAUUZWI


**TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**

Desai Road, off Thika Rd.
S.L.P 30231-00100 Nairobi, Kenya.
Nambari ya simu: +254(020)3749900-9, 3748204, 3747994
Kipepesi: +254(020)3639130
Baruapepe: info@kicd.ac.ke, Tovuti: www.kicd.ac.ke